**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

# MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA RUZUKU YA MBOLEA KWA MSIMU WA 2022/2023

**AGOSTI, 2022**

# YALIYOMO

**YALIYOMO** ii

**DIBAJI** iv

**1.UTANGULIZI** 1

1.1 LENGO LA RUZUKU 1

1.2 AINA ZA MBOLEA 1

1.3 MFUMO UTAKAOTUMIKA 2

**2.MADHUMUNI YA MWONGOZO** 2

**3.NGAZI ZA UTEKELEZAJI** 2

3.1. WIZARA YA KILIMO 2

3.2. MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA (TFRA) 3

3.3. KAMATI YA TAIFA YA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA RUZUKU YA MBOLEA 5

3.4. SEKRETARIETI ZA MIKOA 6

3.5. MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA 7

3.6. WAINGIZAJI/ WAZALISHAJI WA MBOLEA 8

3.7. MAWAKALA (*AGRODEALERS*) WA MBOLEA 9

3.8. TAASISI ZA FEDHA 9

3.9. WAKULIMA 10

**4.JINSI MFUMO UTAKAVYOFANYA KAZI** 10

**5.MAMBO YA KUZINGATIWA** 13

5.1 UTAMBUZI WA WAINGIZAJI/WAZALISHAJI WA MBOLEA YA RUZUKU 13

5.2 UTAMBUZI WA MAWAKALA WA MBOLEA (WANAOUZA KWA WAKULIMA) 14

5.3 UTAMBUZI WA WAKULIMA 14

5.4 UPATIKANAJI, USAMBAZAJI NA UUZAJI WA MBOLEA 15

5.5 ULIPAJI WA FEDHA ZA RUZUKU 16

5.6 MWISHO WA MATUMIZI YA RUZUKU YA MBOLEA 16

**6.UFUATILIAJI NA TATHIMINI** 17

**7.UTARATIBU WA KUPOKEA NA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO** 17

7.1 MALALAMIKO YA WADAU 17

7.2 MALALAMIKO YANAYOHUSU MALIPO NA MFUMO WA KIDIJITALI 17

**8.HITIMISHO** 18

# DIBAJI

Katika msimu wa 2022/2023, Serikali imepanga kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima kwa lengo la kupunguza gharama ya mbolea kwa mkulima ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwanda vya ndani. Utoaji wa ruzuku utazingatia mahitaji halisi ya mkulima kulingana na taarifa za usajili na bajeti ya Serikali iliyotengwa.

Mbolea zitakazohusika kwenye ruzuku ni mbolea za kupandia na kukuzia ambapo DAP kwa ajili ya kupandia na Urea kwa ajili ya kukuzia ambazo ni takribani 50% ya matumizi ya mbolea nchini. Mbolea za kupandia na kukuzia za aina zingine zitahusika kwenye ruzuku kulingana na mahitaji ya soko. Aidha, ili kuhamasisha matumizi ya mbolea zinazozalishwa nchini, mbolea zinazozalishwa na viwanda vya ndani zitaingia kwenye mpango wa ruzuku kulingana na mahitaji ya soko.

Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (*Tanzania Fertilizer Regulatory Authority*-TFRA) itatumia mfumo wa kielektroniki katika kutoa ruzuku ya mbolea kwa lengo la kuongeza kuongeza ufanisi wa utoaji wa ruzuku, kupunguza mianya ya udanganyifu na gharama za usimamizi. Mfumo huo utatumia programu maalum ya kidigitali kusajili wakulima,

wasambazaji/wazalishaji, mawakala pamoja na kuratibu usambazaji wa mbolea kwa wakulima na malipo ya mbolea ya ruzuku.

Utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea utahusisha wadau mbalimbali wakiwemo Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Sekeretariti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Waingizaji/Wazalishaji wa Mbolea, Mawakala (*Agrodealers*) wa Mbolea, Taasisi za Fedha, Wakulima na wadau wengine muhimu.

Mwongozo huu umeandaliwa kwa lengo la kutoa maelekezo ya utaratibu wa utoaji na usimamizi wa ruzuku ya mbolea ikiwa ni pamoja na kuainisha ngazi za utekelezaji na wajibu wa kila wadau katika usimamizi wa ruzuku ya mbolea kwa msimu wa 2022/2023.

## 1. UTANGULIZI

### 1.1 LENGO LA RUZUKU

Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Serikali imepanga kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima nchini. Mpango wa ruzuku unalenga kupunguza gharama ya mbolea kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwanda vya ndani. Ruzuku itatolewa kwa wakulima waliosajiliwa kupitia daftari maalum ngazi ya Kijiji na kuingizwa kwenye mfumo wa kieletroniki ili kuongeza ufanisi na kupunguza mianya ya ubadhirifu.

### 1.2 AINA ZA MBOLEA

Mbolea zitakazohusika kwenye ruzuku ni mbolea za kupandia na kukuzia zikiwemo DAP, Urea na nyinginezo kulingana na mahitaji ya soko. Vile vile, ili kuhamasisha matumizi ya mbolea zinazozalishwa nchini, mbolea zinazozalishwa na viwanda vya ndani zitaingia kwenye mpango wa ruzuku kulingana na mahitaji ya soko. Aidha, kwa mbolea ambazo zitaingizwa nchini kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi (*re-export*) na mbolea zitakazoingizwa kwa ajili ya kutumika kama malighafi hazitakuwa sehemu ya mpango wa ruzuku.

## 1.3 MFUMO UTAKAOTUMIKA

Mfumo utakaotumika kutekeleza mpango wa ruzuku ya mbolea katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 ni wa kielektroniki utakaotumia programu maalum ya kidigitali (*Digital Platform*) kuratibu utekelezaji wa mpango wa ruzuku. Kupitia mfumo huo, wadau muhimu wakiwemo wakulima, waingizaji na wazalishaji wa mbolea, mawakala wa uuzaji wa mbolea watasajiliwa. Aidha, mfumo utaratibu takwimu za usambazaji (*stock movement*); mauzo na malipo kwa watoa huduma wa mbolea ya ruzuku.

## 2. MADHUMUNI YA MWONGOZO

Madhumuni ya mwongozo huu ni yafuatayo:-

(i) Kueleza utaratibu wa usimamizi wa ruzuku ya mbolea; na

(ii) Kuainisha ngazi za utekelezaji na wajibu wa wadau katika usimamizi wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa msimu wa 2022/2023.

## 3. NGAZI ZA UTEKELEZAJI

Utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea utahusisha ngazi mbalimbali zenye majukumu kama ifuatavyo:-

### 3.1. WIZARA YA KILIMO

Majukumu ya Wizara ya Kilimo yatakuwa ni:-

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia mpango wa ruzuku ya mbolea;
(ii) Kufuatilia upatikanaji wa fedha za ruzuku;
(iii) Kuunda Kamati ya Taifa ya Uendeshaji wa utaratibu wa ruzuku ya mbolea (*National Fertilizer Subsidy Steering Committee)*;
(iv) Kutoa Mwongozo wa Utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku;
(v) Kutoa maelekezo yatakayowezesha utekelezaji wa mpango wa ruzuku;
(vi) Kushughulikia masuala mengine yatakayohitaji maamuzi ya Wizara; na.
(vii) Kuhakikisha mpango wa ruzuku unatekelezwa kwa mujibu wa Mwongozo huu.

## 3.2. MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA (TFRA)

Majukumu ya TFRA yatakuwa ni:-

(i) Kusajili wakulima watakaonufaika na ruzuku ya mbolea kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(ii) Kusimamia utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea;
(iii) Kuunda kamati ndogo za kitaalam kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea kwa kadri itakavyohitajika;

(iv) Kuandaa makisio ya mahitaji ya mbolea kwa mikoa yote ya Tanzania Bara;

(v) Kuingia mikataba ya makubaliano na makampuni ya mbolea yaliyosajiliwa kwa ajili ya kuuza mbolea ya ruzuku kwa wakulima;

(vi) Kuingia mikataba na watoa huduma wa mfumo wa kidigitali utakaotumika katika utekelezaji wa ruzuku ya mbolea;

(vii) Kupanga na kutangaza bei elekezi ya mbolea;

(viii) Kushirikiana na wadau wa mbolea katika kufanikisha utoaji wa ruzuku;

(ix) Kuutangazia umma kuhusu kampuni na mawakala wa mbolea waliosajiliwa kuuza mbolea kwa uratibu wa ruzuku;

(x) Kutoa elimu kwa umma kuhusu utaratibu wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine muhimu;

(xi) Kufungua na kusimamia akaunti maalum zitakazotumika kupokea na kulipa fedha za ruzuku kwa watoa huduma;

(xii) Kuidhinisha malipo ya ruzuku ya mbolea iliyouzwa kwa wakulima;

(xiii) Kushirikiana na Taasisi za Fedha kufanya usuluhishi wa malipo ya ruzuku ya mbolea mara kwa mara;

(xiv) Kupokea na kushughulikia malalamiko/changamoto za utekelezaji zinazohusu mpango wa ruzuku ya mbolea na kuwasilisha taarifa Wizara ya Kilimo;

(xv) Kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima; na

(xvi) Kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa Mpango wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa kila mwezi. Aidha, taarifa hizo zitawasilishwa Wizara ya Kilimo na kwenye Kamati ya Taifa ya Uendeshaji wa utaratibu wa ruzuku ya mbolea.

## 3.3. KAMATI YA TAIFA YA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA RUZUKU YA MBOLEA

Kamati ya Taifa ya Uendeshaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea (*National Fertilizer Subsidy Steering Committee)* itakuwa na wajumbe wafuatao:-

- Waziri wa Kilimo
- Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo
- Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango
- Katibu Mkuu wa OR- TAMISEMI
- Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya CRDB PLC
- Mkurugenzi Mkuu wa Vodacom Tanzania PLC

- Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya NMB PLC
- Mkurugenzi wa Sera na Mipango – Wizara ya Kilimo
- Mkurungenzi wa Idara ya Maendeleo ya Mazao – Wizara ya Kilimo
- Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA

Majukumu ya Kamati ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ruzuku yatakuwa:-

(i) Kuidhinisha vigezo vitakavyotumika kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima;
(ii) Kuhakikisha kuwa mpango wa ruzuku ya mbolea unapata fedha na zinatolewa kwa wakati;
(iii) Kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji mpango wa ruzuku ya mbolea; na
(iv) Kutoa maelekezo mahsusi kwa ajili ya kufanikisha lengo la Serikali la utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima.

## 3.4. SEKRETARIETI ZA MIKOA

Majukumu ya Sekretarieti za Mikoa yatakuwa ni:-

(i) Kusimamia Halmashauri zote zilizopo kwenye mikoa husika ili zitekeleze kwa ufanisi majukumu

yake kwa mujibu wa mwongozo wa mpango wa ruzuku;

(ii) Kushirikiana na TFRA katika kuhamasisha na kusajili wakulima ikiwa ni pamoja na kuhakiki kanzidata ya wakulima waliosajiliwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea; na

(iv) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea kila mwezi na kuiwasilisha Wizara ya Kilimo na TFRA.

## 3.5. MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA

Majukumu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yatakuwa ni:-

(i) Kusajili na kuandaa kanzidata ya wakulima katika ngazi ya kijiji/mtaa;

(ii) Kusimamia utoaji wa mbolea ya ruzuku kwa bei zitakazotangazwa na Serikali;

(iii) Kutoa elimu kuhusu kanuni za kilimo bora kulingana na ikolojia ya mazao kwa eneo husika;

(iv) Kusimamia matumizi sahihi ya mbolea ya ruzuku kwa wakulima ili kuhakikisha kuwa mbolea inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa; na

(v) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea kila mwezi na kuiwasilisha ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

### 3.6. WAINGIZAJI/ WAZALISHAJI WA MBOLEA

Kampuni zinazojihusisha na uingizaji na uzalishaji wa mbolea zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

(i) Kuingiza au kuzalisha mbolea zitakazouzwa kwa bei ya ruzuku kwa wakulima;

(ii) Kuteua na kuwasilisha TFRA taarifa za mawakala wa pembejeo watakaoshiriki kuuza mbolea ya ruzuku kwa wakulima;

(iii) Kuingia mikataba na wafanyabiashara/mawakala watakaonunua na kusambaza mbolea ya ruzuku kwa niaba ya kampuni na nakala za mikataba husika ziwasilishwe TFRA;

(iv) Kuweka kwenye mfumo wa kielektroniki taarifa za mbolea iliyozalishwa/kuingizwa nchini na kusambazwa kwenye vituo vya mauzo au kuuzwa kwa wakala;

(v) Kuhakikisha kuwa mfuko wa mbolea ya ruzuku umeandikwa MBOLEA YA RUZUKU na una *QR code* iliyotolewa na TFRA;

(vi) Kuwasimamia mawakala waliowateua ili kuhakikisha wanafikisha na kuuza mbolea ya ruzuku kwa wakulima; na

(vii) Kuwasilisha hati za madai ya fedha za ruzuku kwa TFRA baada ya mbolea kuuzwa kwa mkulima.

## 3.7. MAWAKALA (*AGRODEALERS*) WA MBOLEA

Majukumu ya Mawakala (*Agrodealers*) wa mbolea yatakuwa ni:-

(i) Kuuza mbolea ya ruzuku kwa mkulima aliyesajiliwa kwa mfumo wa ruzuku;
(ii) Kuingiza namba ya utambulisho wa mkulima kwenye mfumo ili kutambua mkulima aliyesajiliwa kunufaika na ruzuku ya mbolea;
(iii) Kuskani *QR code* ya mfuko wa mbolea wakati wa mauzo kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi za mauzo; na
(iv) Kuhakikisha upatikanaji wa mbolea ya ruzuku wakati wote wa msimu wa 2022/2023.

## 3.8. TAASISI ZA FEDHA

Majukumu ya Taasisi za Fedha yatakuwa ni:-

(i) Kupokea fedha za ruzuku ya mbolea kutoka Serikalini kupitia akaunti maalum kwa ajili ya kuwezesha malipo yanayostahili;
(ii) Kufanya malipo kwa kampuni za mbolea zilizotoa huduma ya ruzuku kwa wakulima baada ya kupata idhini ya TFRA;
(iii) Kushirikiana na TFRA kufanya usuluhishi wa malipo ya mbolea ya ruzuku mara kwa mara; na

(iv) Kutoa taarifa ya malipo ya fedha za ruzuku kwa TFRA kila wiki na mwezi.

### 3.9. WAKULIMA

Majukumu ya wakulima watakaonufaika na ruzuku ya mbolea yatakuwa ni:-

(i) Kuhakikisha kuwa amesajiliwa kwenye mfumo kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kupewa namba maalaum ya utambulisho;
(ii) Kuonyesha namba ya utambulisho aliyopewa wakati wa usajili anapokwenda kununua mbolea ya ruzuku;
(iii) Kununua mbolea ya ruzuku kwa bei ya mkulima iliyotangazwa na Serikali; na
(iv) Mkulima haruhusiwi kuuza mbolea ya ruzuku.

## 4. JINSI MFUMO UTAKAVYOFANYA KAZI

Utekelezaji wa utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima utazingatia utaratibu ufuatao:-

4.1. Kampuni zitaingiza/kuzalisha mbolea nchini na kuifungasha katika mifuko yenye uzito wa kilo 25 na 50 ambayo imeandikwa "MBOLEA YA RUZUKU" na imechapwa *QR code* itakayotolewa na TFRA;
4.2. Makampuni yatasambaza mbolea kwenye vituo vya mauzo na mawakala na zoezi hilo litahusisha utoaji na upokeaji wa mzigo kwenye mfumo (*stock check*

*out and in*) kati ya kampuni na kituo cha mauzo au wakala;

4.3. Makampuni yatabainisha na kuwasilisha majina ya mawakala waliosajiliwa ambao watasambaza mbolea ya ruzuku;

4.4. Mkulima aliyesajiliwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (*Local Government Authority* - LGAs) ataenda kwa mfanyabiashara/wakala wa mbolea aliyesajiliwa kwa ajili ya kununua mbolea na kuonyesha namba ya utambulisho aliyopewa wakati wa usajili;

4.5. Mfanyabiashara ataingiza namba ya utambulisho wa mkulima kwenye mfumo na kuhakiki taarifa zake kabla ya kumuuzia mbolea;

4.6. Mkulima atafanya malipo ya mbolea kwa mfanyabiashara/wakala kwa kuzingatia bei iliyotangazwa na Serikali;


4.7. Baada ya mkulima kufanya malipo, mfanyabiashara/wakala ataskani *QR code* ya mfuko wa mbolea iliyouzwa na taarifa za mbolea hiyo (aina, kampuni na namba ya mfuko) zitaingia kwenye mfumo wa ruzuku;

4.8. Taarifa za mauzo zitaonekana kwa kampuni husika na TFRA;

4.9. Kampuni itawasilisha TFRA hati ya madai kwa kiasi cha mbolea ambacho kimeuzwa kwa mkulima;

4.10. TFRA itaidhinisha malipo ya fedha ya ruzuku kwa kampuni husika kwa muda usiozidi siku kumi na nne;

4.11. Taasisi za fedha zitafanya malipo kwa kampuni iliyouza mbolea ya ruzuku baada ya kupata idhini kutoka TFRA (**Kielelezo Na. 1**).




**Kielelezo Na. 1:** Muundo wa Mfumo wa Ruzuku ya Mbolea

## 5. MAMBO YA KUZINGATIWA

### 5.1 UTAMBUZI WA WAINGIZAJI/WAZALISHAJI WA MBOLEA YA RUZUKU

Usajili wa kampuni za mbolea ya ruzuku utafanywa na TFRA kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

5.1.1 Mwombaji atatakiwa kuwasilisha taarifa zifuatazo:-

(i) Jina la kampuni;
(ii) Kituo/vituo vya mauzo (mkoa, wilaya, kijiji);
(iii) Cheti cha usajili wa kampuni kutoka BRELA;
(iv) Namba ya utambulisho wa mlipa kodi;
(v) Namba ya simu;
(vi) Namba ya leseni ya kufanya biashara ya mbolea;
(vii) Namba ya akaunti itakayotumika katika benki iliyokubalika; na
(viii) Aina na kiasi cha mbolea atakayouza kwenye mfumo wa ruzuku.

5.1.2 TFRA itachambua wa maombi na kutoa mrejesho kwa mwombaji ndani ya siku 14; na

5.1.3 Iwapo muombaji atakuwa amekidhi vigezo atasajiliwa na kupewa namba maalum ya utambulisho.

## 5.2 UTAMBUZI WA MAWAKALA WA MBOLEA (WANAOUZA KWA WAKULIMA)

Usajili wa mawakala utafanywa na TFRA na utahusisha:-

5.2.1 Mawakala watakaoteuliwa na kampuni (waingizaji/wazalishaji) kwa ajili ya kusambaza na kuuza mbolea za ruzuku;

5.2.2 Taarifa zitakazohitajika kwa ajili ya usajili wa mawakala wa mbolea za ruzuku ni pamoja na:-

- (i) Jina la kampuni au mfanyabiashara;
- (ii) Kituo/vituo vya kutoa huduma (mkoa, wilaya, kijiji);
- (iii) Namba ya utambulisho wa mlipa kodi;
- (iv) Namba ya simu;
- (v) Namba ya leseni ya kufanya biashara ya mbolea;
- (vi) Aina na kiasi cha mbolea atakayo shiriki kufanya biashara.

5.2.3 TFRA itachambua maombi na kutoa mrejesho kwa mwombaji ndani ya siku 14.

5.2.4 Iwapo mwombaji atakidhi vigezo atasajiliwa na kupewa namba maalum ya utambulisho.

## 5.3 UTAMBUZI WA WAKULIMA

Usajili wa mkulima mmoja mmoja, vyama vya ushirika na kampuni zinazoendesha kilimo cha mashamba makubwa (*estates*) utafanywa na  Mamlaka za Serikali za mitaa kwa utaratibu ufuatao:-

(i) Afisa ugani atafanya usajili wa wakulima katika ngazi ya kijiji kwa kutumia fomu maalum (TFRA/1);
(ii) Taarifa za usajili zitakuwa kama ilivyoainishwa kwenye fomu namba TFRA/1;
(iii) Afisa mtendaji wa kijiji/mtaa atathibitisha taarifa za usajili kwenye fomu;
(iv) Afisa ugani ataingiza taarifa za usajili kwenye mfumo; na
(v) Mkulima mnufaika aliyesajiliwa atapewa namba maalum ya utambulisho ambayo ataitumia anapoenda kununua mbolea kwa wakala.

## 5.4 UPATIKANAJI, USAMBAZAJI NA UUZAJI WA MBOLEA

Utaratibu wa upatikanaji, usambazaji na uuzaji wa mbolea ya ruzuku utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Mwingizaji/Mzalishaji wa mbolea aliyesajiliwa na TFRA na kusaini mkataba atawajibika kuingiza/kuzalisha mbolea nchini;
(ii) Mwingizaji/Mzalishaji ataingiza kwenye mfumo taarifa za aina na kiasi cha mbolea ya ruzuku kilichoingizwa/kuzalishwa;
(iii) TFRA itatoa *QR code* zinazoendana na kiasi cha mbolea kitakachofungashwa;
(iv) Mwingizaji/Mzalishaji atafungasha mbolea katika mifuko yenye uzito wa kilo 25 au 50 ambayo

imeandikwa "MBOLEA YA RUZUKU" na imechapwa *QR code*;

(v) Mwingizaji/Mzalishaji atasambaza mbolea kupitia vituo vya mauzo na mawakala;

(vi) Mwingizaji/Mzalishaji ataingiza kwenye mfumo taarifa za aina na kiasi cha mbolea iliyotoka au kuuzwa kwa wakala;

(vii) Wakala ataingiza kwenye mfumo taarifa za aina na kiasi cha mbolea kilichopokelewa, kutolewa na/au kuuzwa; na

(viii) Wakala ataskani *QR code* baada ya kuuza mbolea kwa mkulima.

## 5.5 ULIPAJI WA FEDHA ZA RUZUKU

(i) Baada ya kuskani *QR code*, taarifa za mauzo zitaonekana kwa Kampuni husika ya mbolea na TFRA;

(ii) Kampuni itawasilisha hati ya madai kwa TFRA kwa mbolea yake ambayo imeuzwa; na

(iii) TFRA itaidhinisha malipo ya fedha ya ruzuku kwa Kampuni husika kwa muda usiozidi siku kumi na nne (14) baada ya kupokea hati ya madai.

## 5.6 MWISHO WA MATUMIZI YA RUZUKU YA MBOLEA

Utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima kwa msimu wa 2022/2023 itafika ukomo tarehe 30 Juni, 2023.

## 6. UFUATILIAJI NA TATHIMINI

Ufuatiliaji na tathmini utafanywa na Wizara ya Kilimo, TFRA, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kulingana na majukumu yaliyoainishwa kwa kila ngazi ya mamlaka zilizoainishwa kwenye mwongozo huu.

## 7. UTARATIBU WA KUPOKEA NA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO

### 7.1 MALALAMIKO YA WADAU

Malalamiko ya wadau yatawasilishwa na kushughulikiwa kulingana na ngazi za utekelezaji kuanzia Kijiji, Wilaya, Mkoa, TFRA na Wizara.

### 7.2 MALALAMIKO YANAYOHUSU MALIPO NA MFUMO WA KIDIJITALI

Malalamiko yanayohusu malipo na mfumo wa kidijitali yatawasilishwa TFRA kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA),
Barabara ya Mandela,
Kitalu Na. 15471, Mtaa wa 1 Kilimo, Jengo la Kilimo I,
S. L. P. 46238,
**DAR ES SALAAM.**
Simu: +255 222 861 939
Barua pepe: ruzuku@tfra.go.tz

## 8. HITIMISHO

Serikali imeamua kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima ili waweze kununua mbolea kwa bei nafuu na kuwawezesha kuongeza uzalishaji na tija, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza kipato cha wakulima. Hivyo basi, ni wajibu wa wadau wote kutekeleza majukumu yao kikamilifu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Serikali inahimiza ushirikiano wa wadau katika ngazi zote ili kuhakikisha kuwa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea unatekelezwa kwa ufanisi. Mwongozo huu unaweza kufanyiwa maboresho kulingana na mahitaji kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa mpango wa ruzuku.